

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU, MOSHI

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA YA VIWANDA VYA MISITU
KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022**

Mkuu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu kilichopo Moshi Mjini, Mkoani Kilimanjaro anakaribisha maombi ya kujiunga na chuo kwa kozi za Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

1. Kozi zinazotangazwa:

- (i) Astashahada ya Awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level 4) Mafunzo ya mwaka mmoja (1);
- (ii) Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level) Mafunzo ya mwaka mmoja; (1);
- (iii) Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level) Mafunzo ya mwaka mmoja (1);

2. Sifa za mwombaji:

(i) Astashahada ya awali ya teknolojia ya Viwanda vya Misitu;

- (a)** Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari na ufaulu wa alama **D** katika masomo manne;
- (b)** Masomo mawili kati ya hayo aliyofaulu yawe aidha Biolojia au Kemia au Fizikia au Hesabu au Jiografia na masomo mengine mawili kati ya hayo aliyofaulu yasiwe ya dini.
- (c)** Ufaulu wa somo la kiingereza utakuwa kipaumbele cha ziada katika uchaguzi.

(ii) Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu;

Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au Astashahada ya awali ya Ufugaji Nyuki au fani nyingine inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE);

AU

Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya juu ya sekondari na awe na amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu katika masomo mawili kwa alama ya **E** na **S**;

(iii) **Stashahada ya Teknolojia ya Misitu;**

Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au fani nyingine ya sayansi inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE);

4 Jinsi ya Kutuma maombi:

- (i) Mwombaji atatakiwa kujaza fomu, kusaini na kuituma fomu ya maombi ikiwa na vielelezo vyote muhimu;
- (ii) Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi au kwenye tovuti ya chuo [<http://www.fiti.ac.tz>];
- (iii) Maombi yote ya ambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi na taarifa za matokeo katika lugha ya Kiingereza. Endapo mwombaji atakuwa na Ufadhiri, uthibitisho wa maandishi kuhusu Ufadhiri huo utahitajika;
- (iv) Ada ya maombi ya kujiunga na chuo ni Shilingi za Kitanzania **10, 000.00** (elfu kumi) kwa Watanzania na Dola za Kimarekani **20.00** kwa wasio Watanzania;
- (v) Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi kupitia **control number**,
- (vi) Ili kupata **control number** au kupata ufafanuzi wa jinsi ya kujiunga na chuo, mwombaji awasiliane na Afisa udahili wa chuo kwa namba +255752 206 305 au +255755771852
- (vii) Anwani ya kutuma maombi;
Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo:-
admission@fiti.ac.tz au info@fiti.ac.tz au Afisa Udahili, **S.L.P 1925 MOSHI**

5 Tahadhari

- (i) Kwa yeyote ambaye hatazingatia utaratibu uliotajwa hapo juu, maombi yake hayatafikiliwa. Aidha , mwombaji atakayewasilisha hati za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ;
- (ii) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08 September 2021**;

6 Taarifa kwa watakoachaguliwa;

Majina ya wataochaguliwa pamoja na maelezo ya kujiunga na chuo yatawekwa kwenye tovuti ya Chuo (<http://www.fiti.ac.tz>);